ASILEGEE MOYOWE-TRADITIONAL (ME&KE)

1. Asilegee moyowe, asitoke machozi,
   Akimkumbuka Munguwe, kwa yake makombozi,
   Mtoa roho msalabani, mtaka kufa mwenyewe,
   Kwa sababu kumpenda ni, nani mfunga moyowe?

2. Bustani mle Getsemani, amwomba Mungu Baba,
   Je mtu Mungu ana nini?, nguvu zake ni haba,
   Bwana wangu waziona, dhambi za binadamu,
   Mwili wako umetona, kama jasho la damu.

3. "Salamu Rabi salamu", anena Yuda mbaya,
   Mwenye moyo wake mgumu, ambusu pasi haya,
   Aliwaambia “basi, ntakayembusu ndiye,
   Mtwaeni na kwa upesi”, Yuda nani nisiye.

4. Yuda nani siyo yeye, aliyetenda dhambi?
   tukimkosa Mungu baba, kumdharau na Mwana,
   Tukimsikitisha Roho, tu vipofu kama Yuda,
   Tunatupa ne’ma yake, itokayo kwa Yesu

5. Wote ni kupiga mbio, mitumewe pamoja,
   Wamtia mikono yao, askari walokuja,
   Wampeleka hukumuni, aamuliwe na watu,
   Mwenye kutoka uwinguni, Mwam(u)zi mkuu wa watu.

6. Mtume Petro amkanusha, amesema “simjui”,
   Uhodari umekwisha, machoye hainui,
   Pilato amwona Rabbi, hakukosa hata neno,
   Asema “sioni dhambi”, lakini ni mwoga mno.

7. Hathubutu kumwachia, “si hukumu” aomba,
   “Mmoja nitamfungulia, Yesu au Baraba,
   Wayahudi mwamtakani?", “Baraba aachwe tu,
   Yesu afe msalabani, damuye juu yetu”